

## Jinsi ya kuzuia maambukizi ya kifua kikuu kwa watoto

- Watoto wadogo kupatiwa chanjo ya BCG mara wanapozaliwa
- Kugundua na kutibu mapema wagonjwa wa kifua kikuu (watoto na watu wazima) mashuleni na kwenye kaya
- Kutumia dawa ya kuzuia kifua kikuu kwa watoto chini ya miaka mitano wanaoishi na mtu mwenye kifua kikuu
- Kutumia dawa ya kuzuia kifua kikuu kwa watoto wanaoishi na VVU
- Kuishi kwenye nyumba yenye mzunguko mzuri wa hewa
- Kufunika mdomo na pua wakati wa kukohoa
- Kutotema makohozi na mate ovyo



Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia,  
Wazee na Watoto



Kwa maelezo zaidi wasiliana na  
mtoa huduma wa / za Afya aliye karibu nawe.

Kimetolewa na:

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia,  
Wazee na Watoto

kupitia

Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Kifua  
Kikuu na Ukoma

S.L.P. 9083, Dar es Salaam, Tanzania.

Barua pepe: [info@moh.go.tz](mailto:info@moh.go.tz),

Tovuti: [www.ntlp.go.tz](http://www.ntlp.go.tz),

Toleo la 2016

# ELIMU KUHUSU UGONJWA WA KIFUA KIKUU (TB) KWA

# WATOTO



## **Kifua Kikuu ni nini?**

Kifua kikuu ni ugonjwa wa kuambukiza unaosababishwa na vimelea aina ya bakteria visivyoonekana kwa macho ya kawaida bali kwa kutumia hadubini. Kuna aina mbili za kifua kikuu; kinachoshambulia mapafu na nje ya mapafu kama mifupa. Kifua kikuu cha mapafu ndio chanzo cha maambukizi.

## **Mtu anaambukizwaje kifua kikuu?**

Mtu anambukizwa kifua kikuu kwa njia ya hewa kutoka kwa mgonjwa wa kifua kikuu ambaye hajaanza tiba, anapokohoa au kupiga chafya hutoa vimelea ambavyo husambaa kwenye hewa na iwapo mtu mwingine asiye na ugonjwa huu akivuta hewa hiyo anaweza kuambukizwa.

## **Watoto wanaambukizwaje kifua kikuu?**

Kama ilivyo kwa watu wazima, watoto nao huambukizwa kifua kikuu kwa kuvuta hewa yenye vimelea vya ugonjwa ambavyo vinatoka kwa mtu ambaye anaugua na hajaanza matibabu. Chanzo cha maambukizi kwa watoto ni kutoka kwa mtu mwenye ugonjwa wa kifua kikuu ambaye hajaanza matibabu (mtu mzima au mtoto) ndani ya kaya au shuleni.

Watoto walioko kwenye hatari ya kupata kifua kikuu kuliko wengine ni pamoja na:

- Mtoto anayeishi nyumba moja na mtu aliyegundulika kuwa na kifua kikuu
- Mtoto mwenye umri chini ya miaka mitano
- Mtoto mwenye maambukizi ya VVU
- Mtoto mwenye utapiamlo

## **Zipi ni dalili za kifua kikuu kwa mtoto?**

Dalili za kifua kikuu kwa mtoto ni kama ilivyo kwa watu wazima.

Dalili za TB kwa watoto ni pamoja na:

- Kikohozi kwa wiki mbili au zaidi ambacho hakiponi kwa dawa za antibiotiki
- Homa za mara kwa mara wiki mbili au zaidi ambazo haziponi kwa matibabu kama malaria n.k.
- Kupungua uzito, kutoongezeka uzito au ongezeko la uzito usioridhisha
- Kuchelewa kukua kama vile kutambaa au kutembea
- Mtoto kukosa raha ; kulialia, kunyon'gonyea au kutokucheza

## **Ugunduzi wa kifua kikuu kwa watoto ni upi?**



kifua kikuu kwa watoto kinagundulika kwa kupima sampuli ya makohozi na kupiga picha ya ( X-ray). Hata hivyo ugunduzi au uchunguzi ni mgumu kwa kuwa watoto wenye umri chini ya miaka sita wengi wao hawawezi kutoa makohozi. Pia vimelea vya TB kwenye makohozi ni vichache na hivyo inakuwa vigumu kuonekana kwenye hadubini.

## **Matibabu ya kifua kikuu kwa watoto**

Kwa kifua kikuu cha kawaida matibabu ni miezi 6 mpaka mwaka mmoja kulingana na aina ya kifua kikuu. Kwa kifua kikuu sugu ni miezi 18 mpaka 24.